

**HOTUBA YA MGENI RASMI KUFUNGA
MAFUNZO KWA WATENDAJI KUZUIA
MAAMBUKIZI YA VVU KUTOKA KWA
MAMA MWENYE VVU KWENDA KWA
MTOTO KIPINDI CHA UJAUZITO AU
ANAPONYONYESHA**

Ndugu Mganga Mkuu wa Mkoa,

Ndugu Wakufunzi,

Ndugu Washiriki,

Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa upendo na huruma yake kubwa kwetu kwa kutuwezesha kufika hapa leo hii tukiwa wenye afya kwa shughuli hii muhimu. Ni kwa rehema zake mafunzo haya yameweza kufanikiwa.

Pia napenda kuishukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuendelea kuwa

wasimamizi wakuu kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa kufuata miongozo iliyopo.

Vile vile napenda kuishukuru Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa kupitia Idara ya Afya kuweza kufanikisha mafunzo haya.

Vilevile hatuna budi kuwashukuru wadau wetu wa WRP ambao ndio waliofadhili mafunzo haya. Shukrani za dhati ziwafikie wakufunzi na washiriki ambao mmefika hapa ili kufanikisha mafunzo haya.

Ndugu Washiriki,

Kutokana na tafiti za VVU na Malaria mwaka 2011-2012, kiwango cha maambukizi katika mkoa wa Rukwa kilikuwa 6.2% na kiwango cha maambuzi Kitaifa kilikuwa 5.1%. Takwimu hizi zinaonesha kwamba hali ya maambukizi katika mkoa wetu iko juu sana.

Kuna njia mbalimbali ambazo zinaweza kupelekea kupata maambukizi, mojawapo ikiwa ni

maambukizi ya VVU kutoka kwa mama mwenye VVU na mjamzito wakati wa uchungu na kujifungua au anaponyonyesha.

Mkoa wa Rukwa nao pia hauko nyuma katika kupambana na maambukizi hayo, umekuwa ukitoa huduma mbalimbali ili kuhahakikisha afya ya mama na mtoto inaboreshwa. Sambamba na huduma ya upimaji VVU inayotolewa, bila shaka wale ambao wanabainika wana maambukizi wanaanzishiwa dawa za kupunguza makali ya VVU mara moja.

Hivyo basi, ninyi watendaji nategemea mtakuwa wawakilishi wazuri wa Serikali kwa utendaji unaoendana na utaratibu uliowekwa na utendaji wenye tija kwa afya kwa wale wanaopata huduma hiyo bila unyanyapaa wa aina yoyote.

Ndugu Washiriki,

Ili kupunguza kiwango cha maambukizi ya VVU hapa katika Mkoa wetu wa Rukwa yapo masuala mnapaswa kufanyia kazi na kusimamia kwa karibu. Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na:-

- (i) Kutoa huduma kwa kufuata miongozo
- (ii) Kutoa elimu ya afya na uzazi kwa akina mama waja wazito na wanaonyonyesha ikiwemo na kuisitiza ushiriki wa akina baba katika masuala ya afya ya uzazi na mtoto
- (iii) Kutoa huduma ya upimaji VVU na kuwaanzishia dawa wale watakaokutwa na maabukizi
- (iv) Kutoa elimu ya ushauri nasaha juu ya ufuasi mzuri wa dawa za kupunguza makali ya VVU. Elimu hii itasaidia wateja wetu waendeleo kutumia dawa bila kuacha na hivyo kuleta matokeo mazuri kwa mama na mtoto
- (v) Kuwachukua vipimo pamoja na kufuatilia majibu kwa watoto watakaokuwa wamezaliwa na akina mama wenye VVU
- (vi) Kuendelea kuwafuatilia watoto wote watakozaliwa na akina mama wenye VVU kufuatana na miongozo iliyopo

- (vii) Kuhakikisha kuwa vitendanishi na dawa zinakuwepo wakati wote katika vituo vya kutolea huduma.

Nina hakika, ikiwa kila mmoja atatekeleza majukumu yake na kuyafanyia kazi yote niliyoyataja pamoja na mengineyo. Natumaini kwamba maambukizi kutoka kwa mama mwenye VVU kwenda kwa mtoto yatapungua kufikia chini ya 5% kama takwimu za kitaifa zinavyohitaji. Ni muhimu mkusanye taarifa sahihi ambazo zitatoa takwimu sahihi zitakazoweza kupanga mipango sahihi. Ili kuweza kufanikiwa ni lazima kila mmoja wenu aweze kufanya kazi kwa bidii na kwa weledi wa hali ya juu.

Ndugu Washiriki,

Napenda nimalizie kwa kusema kwamba watoto wetu kuepuka maambukizi ya Virus Vya Ukimwi inawezekana. Jambo la msingi ni kuhakikisha yale waliyopata katika mafunzo haya yanafanyiwa kazi. Naamini sote kwa pamoja tukishirikiana suala hili linawezekana.

Niwatakie utendaji wa kazi mwema na Heri ya Sikukuu za Krismas na Mwaka Mpya wa 2017. Kwa wale mnaotoka nje ya Manispaa ya Sumbawanga nawatakia safari njema.

Baada ya kusema hayo, sasa natamka kuwa mafunzo ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama mwenye VVU kwenda kwa mtoto kipindi cha ujauzito ama anaponyonyesha yamefungwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Zelote Stephen Zelote
Mkuu wa Mkoa wa Rukwa